TANGAZO LA SERIKALI Na. 24 la tarehe 12/1/2024

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA 413)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45(2)(i))*

KANUNI ZA UWEZESHAJI WA WATOA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA, 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
USAJILI WAWEZESHAJI WA WATOA HUDUMA ZA USAFIRI

4. Utaratibu wa kusajili.
5. Vigezo vya kuomba kusajiliwa.
6. Uamuzi wa maombi na utoaji wa kadi ya usajili.
7. Uhalali wa usajili.

SEHEMU YA TATU
UTOAJI WA USAJILI

8. Ada ya usajili na tozo nyingine.
9. Kuhuisha usajili.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA UWEZESHAJI YA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI
HUDUMA ZA USAFIRI

10. Masharti ya usajili.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA KWA WAWEZESHAJI WA WATOA
HUDUMA ZA USAFIRI

11. Taarifa za mwezeshaji.
12. Mkataba wa huduma.
13. Kuonyesha Kadi ya usajili.
14. Mamlaka ya kusitisha usajili.
15. Utaratibu wa kusitisha.
16. Kufutwa kwa usajili.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA UJUMLA

17. Wajibu wa kutoa taarifa.
18. Makosa na adhabu.
19. Mamlaka ya kukagua.
20. Makatazo.
21. Mapitio.
22. Rufaa.

MAJEDWALI

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA 413)

## KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45(2))*

KANUNI ZA UWEZESHAJI WA WATOA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA, 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uwezeshaji wa Watoa Huduma za Usafiri za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa wawezeshaji wa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo kupitia mifumo, usimamizi au kwa namna yoyote ya uwezeshaji.

Tafsiri

Sura ya 413

**3**.Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"wakala wa basi" maana yake ni mtu au kampuni inayojitegemea ambayo inatoa huduma kwa niaba ya mtoa huduma;

"huduma ya ukusanyaji na usambazaji wa mizigo" maana yake ni huduma inayolipiwa kwa ajili ya kukusanya bidhaa kutoka kwa wateja mbalimbali na kukabidhi kwa mtoa huduma kwa ajili ya huduma za usafirishaji;

"mwezeshaji" maana yake ni mtu au kampuni iliyosajiliwa na Mamlaka ili kuwezesha utoaji wa huduma za usafirishaji kupitia mifumo, usimamizi au kwa namna yoyote ya uwezeshaji;

"mfumo wa leseni" inajumuisha Mfumo wa Usimamizi wa taarifa za barabara na reli au mfumo mwingine wowote unaotumika na Mamlaka kwa dhumuni hilo;

"maombi ya mtandaoni" maana yake ni maombi yanayotumwa kupitia mfumo wa Mamlaka kwa uwezeshwaji wa mtu mwingine;

"mtoa huduma" ni mtu au kampuni inayomiliki chombo cha huduma za usafirishaji ambaye kwa muktadha wa kanuni hizi atawezeshwa kufanya baadhi ya majukumu yake na mwezeshaji;

"rejesta" maana yake ni kitabu kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za taarifa za shughuli zinazofanywa na mwezeshaji;

"Kifaa cha Ufuatiliaji Mwenendo wa Chombo" maana yake ni kifaa kilichowekwa katika chombo kinachodhibitiwa chenye uwezo wa kutuma taarifa kwa muda halisi kwenda kwenye mfumo wa ufuatiliaji mwenendo wa chombo; au

"Mfumo wa Ufuatiliaji Mwenendo wa Chombo" maana yake ni Mfumo wa kupokea, kutunza na kufuatilia muda na mwenendo wa chombo.

## SEHEMU YA PILI
## USAJILI MWEZESHAJI WA MTOA HUDUMA

utaratibu wa usajili

**4**.-(1) Mtu anayekusudia kutoa huduma ya uwezeshaji atapaswa kuomba kusajiliwa kwa Mamlaka kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(2) Mtoa huduma ya uwezeshaji katika Kanuni hizi ni ambaye anatoa huduma za-

(a) kusaidia ukataji wa tiketi mtandaoni;
(b) kusaidia kufanya maombi katika mfumo wa leseni za Mamlaka;
(c) ufungaji wa vifaa vya ufuatiliaji mwenendo wa chombo;
(d) uwakala wa mabasi;
(e) huduma ya ukusanyaji na usambazaji wa mizigo; na

(f) kusaidia katika mfumo mwingine wowote wa Mamlaka;

(3) Maombi ya usajili wa kuwezesha utoaji wa huduma za usafiri yataambatana na nyaraka zifuatazo:

(a) nakala ya leseni halali ya biashara;
(b) nakala ya umiliki wa ofisi au makubaliano ya kukodi;
(c) nakala halisi ya hati safi ya malipo ya kodi; na
(d) nakala ya kitambulisho cha taifa kwa mtu binafsi au cheti cha usajili wa kampuni.

Vigezo vya kuomba usajili

**5**. Mtu anayeomba kusajiliwa chini ya Kanuni hizi atatakiwa kuwa na vifaa, miundombinu au vitendea kazi vilivyoainishwa na Mamlaka kwa ajili ya kutoa huduma anayoiomba.

Uamuzi wa maombi na utoaji wa kadi ya usajili

**6**.-(1) Baada ya kupokea maombi chini ya Kanuni hizi, Mamlaka-

(a) itakubali maombi na kutoa kadi ya usajili; au
(b) itakataa maombi na kumtaarifu mwombaji kwa maandishi ndani ya siku saba za kazi na kutoa sababu ya kukataliwa.

(2) Endapo Mamlaka itaridhia maombi, kadi ya usajili itatolewa chini ya Kanuni hizi ambayo itakua na maelezo yafuatayo:

(a) jina na anwani ya mwezeshaji;
(b) namba ya usajili ya mwezeshaji;
(c) muda wa usajili;
(d) vigezo na masharti kwa mwezeshaji; na
(e) huduma iliyosajiliwa.

Uhalali wa kadi ya usajili

**7**. Kadi ya usajili inayotolewa chini ya Kanuni hizi itakuwa halali kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kutolewa na inaweza kuhuishwa.

## SEHEMU YA TATU
## UTOAJI WA USAJILI

Ada ya usajili na tozo nyingine

**8**. Mtu anayeomba kusajiliwa atatakiwa kulipa ada na tozo nyingine zinazohusiana na maombi kwa Mamlaka kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Kuhuisha kadi ya usajili

**9**.-(1) Mwezeshaji anaweza kuomba kuhuisha usajili ndani ya siku thelathini kabla ya kuisha kwa muda kadi ya usajili.

(2) Maombi ya kuhuisha kadi ya usajili yanapaswa kufanyika kwa kujaza fomu iliyoainishwa chini ya Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(3) Maombi ya kuhuisha usajili wa kadi yatakayofanywa baada ya kuisha muda wa usajili wa kadi yatahusisha malipo ya asilimia hamsini ya ada ya usajili pamoja na asilimia tano ya faini iliyolimbikizwa kwa miezi inayofuata kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili.

(4) Mamlaka haitashughulikia maombi ya kuhuisha usajili wa kadi endapo kuna madeni ya nyuma katika usajili ulioisha.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA UWEZESHAJI WA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

Masharti ya mwezeshaji

**10**.-(1) Mwezeshaji wa huduma za usafirishaji atahakikisha kuwa -

(a) ana kadi halali ya usajili;
(b) anatunza rejesta katika eneo la ofisi;
(c) nembo ya Mamlaka haitumiki kutangaza biashara yake;
(d) haajiri mfanyakazi wa Mamlaka;
(e) hakuna matangazo wala ushawishi kwa wateja unaofanyika hadharani au katika ofisi za Mamlaka;
(f) maeneo ya ofisi, majengo au vitendea kazi vya Mamlaka havitumiki kufanya biashara;
(g) anatoza tozo za huduma zilizoidhinishwa na Mamlaka;

(h) anampatia mtoa huduma nyaraka za maombi, utambulisho wa akaunti pamoja na nywila;
(i) anatumia lugha ya staha kwa wateja;
(j) anatoa stakabadhi halali ya malipo kwa wateja;
(k) wafanyakazi wake wana ujuzi wa huduma wanazozitoa; na
(l) kwa wakala wa mabasi, atatakiwa kuwa na mkataba baina yake na mtoa huduma.

(2) Mwezeshaji wa maombi ya mtandaoni atatakiwa kuhakikisha kuwa maombi ya mtoa huduma yanaifikia Mamlaka ndani ya saa kumi na mbili baada ya kuyapokea.

(3) Vifaa vya ufuatiliaji mwenendo wa chombo vinavyosambazwa kwa watoa huduma vinatakiwa view na ubora stahiki.

(4) Mkusanyaji na msambazaji mizigo atahakikisha kuwa-
(a) bidhaa za mteja zinawasilishwa katika eneo lililokusudiwa kwa kulingana na makubaliano;
(b) bidhaa za mteja zinahifadhiwa vizuri na kwa usalama; na
(c) chombo kinachobeba mizigo kina leseni halali ya Mamlaka.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA YA UWEZESHAJI WA MTOA HUDUMA

Taarifa za mwezeshaji

**11**. Mwezeshaji atapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka taarifa ya mabadiliko yoyote ya taarifa alizojaza wakati wa kufanya maombi ndani ya siku saba tangu tarehe ya mabadiliko hayo.

Mkataba wa huduma

**12**. Mwezeshaji atapaswa kuingia mkataba wa huduma na mtoa huduma na kuhakikisha kuwa anatunza makubaliano hayo na kuyatoa pale yanapohitajika.

Kuonesha kadi ya usajili

**13**. Mwezeshaji atahahakisha kuwa ana kadi ya usajili inayowekwa katika sehemu ya wazi kwenye ofisi yake kurahisisha ukaguzi.

Mamlaka ya kusitisha usajili

**14**.-(1) Mamlaka inaweza kusitisha usajili, iwapo itajiridhisha kuwa mwezeshaji-

(a) ameshindwa kutoa huduma kama inavyopaswa;
(b) amezuia Afisa wa Mamlaka kufanya ukaguzi;
(c) amekaidi amri halali ya Afisa wa Mamlaka; au
(d) ametenda kosa hilo chini ya Kanuni hizi kwa zaidi ya mara tatu.

(2) Endapo ukiukwaji utahusisha kuvuruga utendaji wa mfumo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa chombo, usajili utasimamishwa kwa muda wa siku tisini.

Utaratibu wa kusitisha usajili

**15**.-(1) Mamlaka kabla ya kusitisha usajili, itatoa notisi kwa mwezeshaji ya kutoa utetezi wa kwanini usajili wake usisitishwe.

(2) Mwezeshaji, baada ya kupokea notisi chini ya kanuni ndogo ya (1), anapaswa kuwasilisha utetezi wake kwamaandishi ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kupokea notisi na kutoa sababu kwanini usajili wake usisitishwe.

(3) Mamlaka inaweza kusitisha usajili na kutoa sababu ya kusitisha iwapo-

(a) Mamlaka haijaridhishwa na utetezi uliowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (2); au
(b) mwezeshaji hajawasilisha utetezi wake.

(4) Endapo usajili umesitishwa chini ya kanuni ya 14, mwezeshaji atapaswa kusitisha utoaji wa huduma ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kusitisha usajili, na atapaswa kukabidhi kadi ya usajili kwa Mamlaka.

(5) Endapo usajili utabaki kuwa halali mpaka kipindi cha kusitisha usajili kitakapoisha, Mamlaka itarudisha kadi ya usajili kwa mwezeshaji baada ya muda wa kusitisha kumalizika na kutekeleza maelekezo mengine kama yalivyoainishwa kwenye notisi ya usitishwaji.

Kufutwa kwa usajili

**16**. Mamlaka itafuta usajili endapo mwezeshaji atakuwa amesitishiwa usajili zaidi ya mara tatu.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA UJUMLA

Wajibu wa kutoa taarifa

**17**. Mwezeshaji atatakiwa kuitaarifu Mamlaka endapo atasitisha huduma zake kwa kipindi kinachozidi siku thelathini.

Makosa na Adhabu

**18**. Mtu atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi anatenda kosa na atakiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo cha kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Mamlaka ya kukagua

**19**. Afisa wa Mamlaka atakuwa na mamlaka ya kukagua huduma zinazotolewa na mwezeshaji ili kujiridhisha kuwa vigezo na masharti ya usajili yanazingatiwa.

Makatazo

**20**.-(1) Mtu ambaye hajasajiliwa na Mamlaka hataruhusiwa kuendesha shughuli za mwezeshaji wa huduma za usafiri ardhini.

(2) Mtu ambaye amesajiliwa kuwa mwezeshaji wa watoa huduma za usafiri ardhini hatoenda kinyume na vigezo na masharti yaliyowekwa kwenye kadi ya usajili.

(3) Kadi ya usajili itakapotolewa haiwezi kuhamishika.

Mapitio
T.S Na. 73 la 2020

**21**. Mtu ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Mamlaka atatuma maombi ya mapitio kulingana na Kanuni za Utaratibu wa Mapitio za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini. .

Rufaa

Sura ya 285

**22**. Mtu ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Bodi chini ya Kanuni hizi anaweza kukata rufaa kwenye Baraza la Ushindani kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya maamuzi.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

### FOMU YA MAOMBI

Weka alama ya vema kwa huduma unayotaka kuwezesha

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Huduma mtandao | | wasaidizi wa huduma zozote za Mamlaka | | Wakala wa huduma za mabasi | |
| Ukusanyaji wa mizigo | | Tiketi mtandao | | Kufunga vifaa vya kudhibiti mwendo | |

A. MAELEZO YA MUOMBAJI WA USAJILI

1. Jina kamili la Muombaji ………...........................................................
   (Jina/Kampuni/Mbia – kwa herufi kubwa)
   Sanduku la Posta …………………………………....………
   Namba ya ofisi: ………………………………..
   Namba ya simu ya muombaji:...………………..
   Nukushi: ………………………………

2. Anwani ya makazi:
   Mtaa: ………………. ……………
   Namba ya kitalu: …………….....
   Namba ya ofisi: ............................
   Namba ya kitalu: …………………

3. Je, una maombi yoyote yaliyokataliwa/ kusitishwa au kufutwa?
   Ndio:……………………………
   Hapana:…………………………
   Ikiwa ni Ndiyo, eleza lini na wapi maombi ya awali yalikataliwa, leseni kusitishwa au
   kufutwa……….......................................................................…………………………
   ………………………………………………………………………………………
   ……….
   Toa sababu ya maombi kukataliwa, kusimamishwa au kufutwa……………………………………………………………………………….
   …..na tarehe ………...............

B. NYARAKA ZA KUTOA KIPINDI CHA MAOMBI

1. Maombi ya kwanza lazima yaambatishwe na vitu vifuatavyo:
   (a) nakala halali ya leseni ya biashara;

(b) nakala ya umiliki wa ofisi au makubaliano ya pango;
(c) cheti cha mlipa kodi;
(d) nakala ya kitambulisho cha Uraia kwa mtu binafsi au cheti cha usajili kwa kampuni; na
(e) ikiwa ni wakala wa basi atapeleka nakala ya makubaliano ya huduma ya muendeshaji;

C. KUHUISHA

Uthibitisho wa malipo ya tozo ya Mamlaka kwa mwaka uliotangulia;

TAMKO

Mimi/ Sisi …………………………………………………………………..………. ninaapa/tunaapa kwamba kwa akili zetu/zangu timamu naamini kuwa taarifa nilizotoa/tulizotoa kwenye maombi haya ni ukweli mtupu.

Jina Kamili ………………………………... Sahihi: ………………………...
Wadhifa: ………………………………. Tarehe: …………………………….

KWA MATUMIZI YA OFISI

Uhakiki na Uidhinishaji

(a) Haijaidhinishwa:
Toa sababu
…………………........……………………………………..

(b) Imeidhinishwa:

Tarehe ya kuanza: ………………….
Tarehe ya mwisho: …………………..
Jina kamili la afisa: ……………………………………….
Cheo: ……………………………….
Sahihi: ……………………………
Tarehe : ……………………………

Kiasi kilicholipwa: ……………….. Namba ya risiti. ……………..

Tarehe :...………………………… Sahihi: ………………………..

NAMBA YA JALADA LA MWENYE LESENI: ………....................................

ONYO:

1. Kujua kuwa kutoa taarifa ya uongo kwa lengo la kujipatia leseni ni kosa linaloadhibiwa na faini au kifungo.

*Tangazo la Serikali Na.24 (Linaendelea.)*

2. Mabadiliko yoyote ya maelezo yaliyotolewa kwenye fomu hii yatawasilishwa kwa Mamlaka, vinginevyo utakuwa umefanya kosa chini ya Kanuni hizi.

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8)*

ADA ZA WAWEZESHAJI

| Na. | MAELEZO | ADA KWA MWAKA (TSHS) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi | 50,000 |
| 2. | Kusaidia maombi ya Mamlaka leseni mfumo | 200,000 |
| 3. | Wakala wa mabasi | 500,000 |
| 4. | Huduma ya ukusanyaji mizigo | 500,000 |
| 5. | Kusaidia mfumo wowote wa Mamlaka | 300,000 |

Dodoma,
15 Disemba, 2023

MAKAME MNYAA MBARAWA,
*Waziri wa Uchukuzi*